



13



14

Maaskofu pale Roma waliona kuwa dhamira hiyo ni kubwa sana: Mti mmoja wa Maristi ukiwa na matawi mengi.

13. Mwishowe Mtakatifu akasema "Ndio" na kukubaliana na wazo la mapadri wa Maristi, mara tu baada ya Baba Jean-Claude kukubali kupeleka watumishi kwa watu wa Visiwa vya Pacifiki.

Baba Jean-Claude alichaguliwa kuwa kiongozi wa Maristi na ndipo alipoahidi yeye pamoja na wenzake kuishi maisha ya Maristi.

14. Baba Jean-Claude akawaaga na kuwaombea mema watumishi wa kwanza waliokwenda katika kazi za utumishi nchi za mbali.

Katika miaka iliyofuatia vijana wengi walijiunga na jamii ya Maristi na Baba Jean-Claude aliweza kuwatuma watumishi wengi zaidi katika nchi za Pacifiki na kuanzisha shule nchini Ufaransa.

15. Mwishoni, Baba Jean-Claude alijivua madaraka na kumpa mtu mwингine ili aweze kutumia muda mwингi katika maombi na shughuri za uhandishi.

Alikwenda kuishi sehemu tulivu nje ya mji ambapo aliendelea kutumia muda mwингi katika kutunga sheria na kanuni za Maristi.

16. Alipokuwa mzee alifariki kwa amani. Leo anakumbukwa kwa upendo mkubwa sana na watu wote wa Maristi akiwa kama ndiyo mwanzilishi na Baba wa jamii.




15



16

Swahili

## Maisha ya Jean-Claude Colin



[www.jeanclaudecolin.org](http://www.jeanclaudecolin.org)

Mwanzilishi wa  
jamii ya Maria

1. Jean-Claude Colin alizaliwa katika kijiji kidogo nchini Ufaransa. Alikuwa na kaka na dada saba. Nyumba ya familia yake ilikuwepo karibu na kilima kidogo nje ya mji.



2. Kwa sababu za kutolewana kati ya Kanisa na serikali mapadri wa Jean-Claude walikuwa wakiwasaidia watumishi wa parokia kwa kuwapa hifadhi dhidi ya watumishi wa serikali.

Wakati mwagine walikuwa wakienda msituni kujificha. Kabla ya Jean-Claude hajatimiza umri wa miaka mitano wazazi wake wote waliumwa sana na kufariki, ikabidi mjomba wake mkarimu amchukue na kumlea yeye pamoja na kaka na dada zake.



3. Jean-Claude alihamia mji wa karibu na kuishi katika pamoja na mjomba wake, karibu sana na kanisa la parokia. Pamoja na kwamba alikuwa ni mtu wa aibu Jean-Claude alikuwa anapenda sana kuwasaidia mapadri katika Misa. Wakati mwagine alikuwa akitumia muda peke yake nje ya mji.



4. Wakati akiwa na miaka kumi na nne Jean-Claude alikwenda katika shule ya bweni. Wavulana wengi pale shulen iwalikuwa na dhamira ya kuwa mapadri. Jean-Claude alistaajabu kama na yeye atakuwa mmoja wapo. Miaka michache ijayo aliendelea katika shule nydingine mbili zaidi. Alikuwa mwanafunzi mzuri ingawa wakati mwagine alikuwa akiumwa mara kwa mara.



5. Hatimaye alikwenda mjini kuendelea na masomo ya upadri. Wazo lilimjia kichwani—kwamba Mama Yetu Mbarekiwa, Maria, alimuomba aanzishe familia mpya katika kanisa.

Jean-Claude alikuwa mmoja kati ya watu kumi na mbili katika kundi ambao waliwaza kuhusu familia hii mpya ambayo ilikuja kuitwa Jamii ya Maria. Ikiundwa na mapadri, na watumishi wa kike na wa kiume, mti na matawi mbalimbali.



6. Siku moja baada ya Jean-Claude kuteuliwa kuwa padri, watu hao kumi na mbili walikwenda katika kanisa dogo na



kupiga magoti mbele ya sanamu ya Maria na Yesu.

Walihaidi kuanzisha jamii ya Maria haraka iwezekanavyo. Jamii hiyo ikapewa jina la 'Marists.'

7. Baada ya hapo, kijana Jean-Claude ambaye sasa ni Baba mtumishi alipelekwa katika kanisa dogo milimani ambapo kaka yake alikuwa ni padri wa hilo kanisa.



Wakazi wa mji huo walikuwa wakilima matunda ya zabibu na kutengeneza mvinyo wa waridi. Kadri Baba Jean-Claude alivyokuja kuwajua na kuwazoea wakazi wa mji huo, aibu ilimuondoka na kuwa ni mtu wa kujiamini.



8. Baba Jean-Claude aliendelea kufikiri sana kuhusu jamii ya Maria na kuomba juu ya taratibu mpya na sheria.



Alituma barua kwa Mtakatifu na kuomba Baraka zake. Mtakatifu alimjibu na kumpa matumaini.

9. Baba Jean-Claude alikuja kumjua askofu vizuri sana na kumuambia kuhusu dhamira yake kuhusu kundi la watumishi wa Maristi.

Askofu alimuarika na baadhi ya wanachama wake wa Maristi waende kuishi katika makiazi ya shule.



Tokea pale waliweza kwenda katika maeneo ya watu wenye shida katika makanisa yaliyopo huko milimani wakiwa kama watumishi wa bwana.



10. Kazi zao za mwanzoni za utumishi zilikuwa katika hari ngumu kwenye milima ya theruji na isiyopitika kwa urahisi.

Baba Jean-Claude na wenzake walileta matumaini na imani kwa wakazi wa maeneo yale.

11. Askofu alimuomba Baba Jean-Claude aiendeshe ile shule. Baada ya hapo Marists ikawa jamii ya walimu na watumishi.

12. Baba Jean-Claude akaja kutembelea kanisa katoriki la Roma kwa ajili ya kupewa ruksa kuhusiana na jamii ya Maria.